



Kwa nini Viboko Hawana Nywele



- ✎ Basilio Gimo, David Ker
- ✑ Carol Liddiment
- ☞ Matteo E. Mwita
- 💬 swahili
- 🔊 nivå 2



Siku moja, Sungura alikuwa akitembea
pembeni ya mto.



Kiboko alikuwepo pia, akitembea huku akila majani mazuri ya kijani.



Kiboko hakumwona Sungura na kwa bahati
mbaya akaukanyaga mguu wa Sungura.
Sungura akaanza kumpigia Kiboko kelele.
“We Kiboko huoni kama umeukanyaga
mguu wangu?”



Kiboko akamwomba Sungura msamaha,
“Samahani, sikukuona, tafadhali nisamehe!”
Lakini Sungura hakukubali na akaendelea
kumbwatukia Kiboko, “Umfanya
makusudi! Kuna siku utakiona, na
nitakulipizia!”

Sungura alienda kumtafuta moto na akamwambia, “Nenda, ukamchome Kiboko akitoka majini kuja kula majani. Alinikanyaga!” Moto ukajibu, “Hakuna tatizo, rafiki yangu Sungura, nitafanya ulichoniomba kufanya.”





Baadaye, Kiboko alikuwa akila majani mbali na mto, aliposhtuka moto umelipuka. Miale ya moto ikaanza kuzichoma nywele za Kiboko.



Kiboko akaanza kulia na kukimbilia kwenye maji. Nywele zake zote zilikuwa zimeungua na moto. Kiboko aliendelea kulia, “Nywele zangu zimeungua na moto! Nywele zangu zote zimeisha! Nywele zangu nzuri!”

Sungura alikuwa na furaha kwa kuwa nywele za Kiboko ziliungua. Hadi leo kwa kuogopa moto, Kiboko hawezi kwenda mbali na maji.





Barnebøker for Norge

barneboker.no

Kwa nini Viboko Hawana Nywele

Skrevet av: Basilio Gimo, David Ker

Illustret av: Carol Liddiment

Oversatt av: Matteo E. Mwita

Denne fortellingen kommer fra African Storybook (africanstorybook.org) og er videreforsmidt av Barnebøker for Norge (barneboker.no), som tilbyr barnebøker på mange språk som snakkes i Norge.

Dette verket er lisensiert under en Creative Commons
[Navngivelse 3.0 Internasjonal Lisens](#).